CHIMBUKO LA ZSSF

ZSSF imeanzishwa kwa Sheria Na. 2 ya mwaka 1998 na kufanyiwa marekebisho kadhaa na kuanzishwa upya kwa Sheria Na. 2 mwaka 2005 baada ya kufanyiwa mapitio makubwa.

Tofauti ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Akiba.
Katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii mwanachama analipwa mafao ya uzeeni kwa kila mwezi tokea tarehe ya kufikia umri wa kustaafu hadi kufariki kwake.

Katika Mfuko wa Akiba mwanachama anarejeshewa ile alioiweka tu, wakati atakapoacha kazi kwa kumaliza mkataba wa ajira, kustaafu au vyenignevyo.

KAZI ZA ZSSF

Kwa kuzingatia kifungu cha 5 cha Sheria ya ZSSF Na. 2 ya mwaka 2005 Mfuko utafanya kazi zifuatazo:-
- Kusajili waajiri wote kuwa wanachama wanufaika na waajiri wote kuwa wanachama wachangiaji.
- Kukusanya michango ya wanachama wake na fedha zote zinazolipwa ZSSF.
- Kuanzisha na kuhifadhi rekodi za kila mwanachama zinazohusu michango yake.
- Kuwekeza fedha zote zinazotokana na michango kwenye miradi yenye faida kama itavyoona Bodi.
- Kufungua na kuendesha hesabu zake za benki kwa mujibu wa masharti yatakayowekwa na Bodi.
- Kulipa mafao kwa wanachama wake au wategemezi wa wanachama wake kulingana na Sheria ya ZSSF.
- Kudhibiti na kuendeleza michango kulingana na maelekezo ua sharia ya ZSSF.
- Kufanya shughuli yoyote ikiwa ni pekee yake au kwa mashirikiano na taasisi nyengine ziwe za Tanzania au popote duniani kwa nia ya kukuza na kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa Hifadhi ya Jamii.

WAJIBU WA MUAJIRI KWA ZSSF

Ni wajibu wa kisheria kwa kila mwajiri kuisajili taasisi yake kuwa mwanachama mchangiaji na kumsajili kila mfanyakazi kuwa mwanachama mnufaika.

Usajili wa Mwajiri ni lazima ufanywe ndani ya siku 14 tokea kuanzishwa kwa taasisi ya muajiriwa kama ilivyobainishwa katika kifungu nambari 17 cha Sheria nambari 2 ya ZSSF ya mwaka 2005.

Aidha mwajiri ana wajibu wa kufanya usajili wa wafanyakazi wake wote ndani ya siku 14 tokea kuanza ajira ya kila mfanyakazi.

Kutokujisajili Mwajiri au kutomsajili mfanyakazi aliye mwajiriwa katika kipindi kilichotajwa ni kosa la kisheria na mwajiri atawajibishwa kwa kutozwa faini, au kifungo cha mwaka mmoja au vyote viliwi.
Kutokana na kifungu nambari 17 cha sheria nambari 2 ya mwaka 2005 inamtaka mwajiri kukata asilimia 7% kutoka katika mshahara wa mfanyakazi wake na yeye kama mwajiri atachangia asilimia 13% kulingana na kima cha mshahara wa mwajiriwa, itakayotimiza asilimia 20% ya kima cha mshahara, kiasi ambacho mwajiri atawasilisha ZSSF ili kumuekea akiba mfanyakazi wake. Kwenda kinyume na agizo hilo ni kosa la jinai na kinyume cha sheria.

Na endapo mwajiri atashindwa kuwasilisha michango ya wafanyakazi wake kwa mujibu wa Sheria kifungu Na. 17 (1) (2) (3) (4) (a) (b) ni kosa la jinai na atapatiwa adhabu ya kulipa faini ya fedha taslim au kifungo kwa kupelekwa jela au adhabu zote mbili kulingana na makosa atakayotiwa hatiani na mahkama. Aidha atatakiwa kulipa michango ambayo hajaiwasilisha katika mfuko.

WAJIBU WA MUAJIRIWA KWA ZSSF

Ni wajibu wa kila muajiriwa kuhakikisha anasajiliwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar na anapewa kitambulisho cha uwanachama.
Kutosajiliwa katika Mfuko kunaweza kusababisha mwanachama kukosa haki zake za msingi kama vile mafao ya kiinua mgongo na pencheni pale atakapofikia umri wa kustaafu ama kupata majanga mbali mbali.
Muajiriwa ana wajibu wa kufuatilia mwenendo wa uwasilishwaji wa michango yake kutoka kwa muajiri wake.
Mwanachama muajiriwa anao wajibu wa kuomba mafao atakapofikia umri wa kustaafu ama kupata majanga kwa kufuata taratibu zilizowekwa kisheria.

AINA ZA WANACHAMA WA ZSSF

ZSSF inayo wanachama kutoka:-
- Wizara na Idara za Serikali.
- Sekta binafsi ambayo hujumuisha Makampuni, Mashirika binafsi, Jumuiya zisizo za kiserikali vikundi vilivyoanzishwa katika sekta isiyo rasmi.
- Mashirika na Makampuni ya Serikali.
- Mtu binafsi aliyejiajiri yeye mwenywe ambae awali aliwahi kuwa mwanachama wa ZSSF.

HAKI ZA MWANACHAMA WA ZSSF

Mwanachama wa Mfuko anayo haki ya kupewa kitambulisho cha uwanachama wa ZSSF.
Aidha mwanachama anayo haki ya kujuwa kiasi cha michango yake katika akaunti za ZSSF. Miongoni mwa haki za mwanachama za ZSSF ni kupewa mafao ya kiinua mgongo na Pencheni.

MAFAO YA ZSSF CHINI YA SHERIA NA. 2 YA MWAKA 2005

Mafao ya uzeeni.
Mafao ya uzeeni hulipwa kwa mwanachama ambaye atafikia umri wa kustaafu kazi kwa hiari (kuanzia umri wa miaka 55 hadi 59 ama kustaafu kwa lazima afikapo miaka 60. Mafao ya uzeeni hujumuisha kiinua mgongo na pencheni ya kila mwezi.

Mafao ya ulemavu

Mafao ya ulemavu hulipwa kwa mwanachama pale ambapo ikitokezea hali itakayomuondoshea uwezo wa kufanya kazi kutokana na ulemavu alioupata. Mafao haya hujuisha kiinua mgongo na pencheni kamili ya kila mwezi iwapo atakuwa amefikia miezi 156 ya uchangiaji katika Mfuko. Akichangia miezi 60 hadi 156 atapata pencheni na kiinua mgongo pungufu.

Mafao ya urithi

Endapo mwanachama atafariki, warithi wake watalipwa mafao ambayo ni kiinua mgongo cha marehemu, kiinua mgongo hiki hujumuisha kiasi chote alichochangia mwanachama pamoja na ziada. Malipo ya mwanachama hulipwa kupitia Afisi Wakala wa Usajili na Biashara na mali ya au Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

Mafao ya Uzazi

Mafao haya yametajwa katika Sheria ya ZSSF yenye lengo la kumkinga mwanachama mwanamke na majanga mbali mbali yatokanayo na uzazi au wakati ambao amekaa nyumbani akimlea mtoto wake mchanga. Mafao haya yatamsaidia mama kuziba pengo la kipato kutokana na kutokuwepo kazini

au kutokana na kutofanya kazi za ziada. Aidha mafao haya hutolewa kwa mwanachama aliyechangia katika Mfuko kwa kipindi kisichopungua miezi thelathini na sita (36) ikiwemo miezi sita ya mwisho mfululizo wakati anaomba fao hiyo.

Mafao ya upotevu wa Ajira

Mafao haya yatalipwa kwa mwanachama aliepoteza ajira kwa kipindi kisichopungua miezi sita (6) na awe raia wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na alipoteza ajira kwa sababu ya kumaliza mkataba ama kuachishwa kazi na mengineyo isipokuwa kwa kuacha kazi kwa hiari yake mwenyewe.

Mafao ya kuumia kazini

Mafao ambayo yatalipwa kwa wafanyakazi walioumia kazini kutokana na ajali wakiwa kazini au maradhi yanayotokana na kazi.

MASHARTI YA ULIPWAJI WA MAFAO

Ili mwanachama aweze kulipwa mafao anatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

- Awe amesajiliwa na kuwa mwanachama mchangiaji wa ZSSF.
- Awe na sababu ya kulipwa mafao kwa mujibu wa Sheria.

Faida za ziada kwa mwanachama:-

- Mafao ya kiinua mgongo ni Zaidi ya kile alichochangia.
- Pia mwanachama huyo hupata pencheni ya kila mwezi hadi kufariki kwake.
- Malipo ya mafao hulipwa mara tu madai ya mafao ya mwanachama yanapokamilika.

Katika kutoa huduma hakuna ubaguzi kwa misingi ya jinsia, ukabila, itikadi au ujimbo.

Maombi ya mafao yote kwa mujibu wa kanuni ya 23 unaelezwa kuhusu maombi ya mafao kama vile kuwasilisha vielelezo muhimu vitakavyohitajika katika taratibu za kudai mafao. Kisha atawasilisha maombi yake katika Ofisi za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii zilizopo karibu nae.

Malipo ya Mafao.

Mkurugenzi Mwendeshaji atafanya malipo ya mafao katika kiwango chochote kwa njia ya hundi ama Benki.

Kuendelea kwa malipo ya Pencheni:-

Katika kuamua kuendelea kwa malipo ya pencheni kwa wanaostahiki, Mfuko utatumia vigezo vifuatavyo:-

- Kujua kwamba iwapo mwanachama yupo hai.
- Mwanachama atatakiwa kufanya uhakiki kila baada ya miezi sita kwa uthibitisho wa kuendelea kumlipa pencheni yake.

Kusita kwa malipo ya pencheni:-

- Malipo ya pencheni yatasita pale tu mwanachama atakapofariki dunia.

Ndugu au familia ya marehemu mwanachama itatakiwa kutoa taarifa kwa ZSSF na kuwasilisha kivuli cha cheti cha kifo na kadi ya ZSSF ya mwanachama.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa:

Mkurugenzi Mwendeshaji
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar
S.LP: 2716 Zanzibar – Tanzania
Simu: +255 24 2230342
Faksi: +255 24 2232820
Barua pepe: info@zssf.or.tz
Tovuti: www.zssf.or.tz
Kilimani Mnara wa Mbao

PEMBA
S.L.P: 293
Simu: +255 24 52050 I Faksi: +255 24 52050
Chakechake
Barua pepe: info@zssf.or.tz
Tovuti: www.zssf.or.tz

MKOA WA KUSINI UNGUJA
S.L.P: 2716, Zanzibar -Tanzania,
Simu: +255 (0)773 232 835,
Barua pepe: info@zssf.or.tz
Tovuti: www.zssf.or.tz
Kitogani

MKOA WA KASKAZINI UNGUJA
S.L.P: 2716, Zanzibar -Tanzania,
Simu: +255 (0)773 336 477,
Barua pepe: info@zssf.or.tz
Tovuti: www.zssf.or.tz
Kinduni

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)



BIDHAA ZA ZSSF